WASIFU, KWA MUKHTASAR WA SHEIKH ‘ALÎ IBN HASAN ‘ABDUL-HAMÎD AL-HALABÎ

Ukoo Wake Na Kunasibika Kwake:

Yeye ni Sheikh wa ki-Salafi, kisha ni mfuasi wa riwaya na mtunzi wa vitabu vingi vya ki-Islamu na vya uswahihishaji, ‘Alî Ibn Hasan Ibn ‘Alî Ibn ‘Abdil-Hamîd Al-Ya’fî, mnasaba wa mahali asiliya atokapo (Jaffa, sehemu ya Kusini-Magharibi mwa Falestina), Al-Halabî, mnasaba wake na (mjini Aleppo, Syria), Al-Urdunî, mnasaba wake na mahali walipotoka jamii yake wakafanya Hijrah na kwenda kuishi (Jordan).

Kuzaliwa Kwake:

Alizaliwa katika Mji wa Zarqâ’, Jordan mnamo 29th, mwezi wa Jumâda ath-Thânî, 1380H.

Babake na babu yake walihamia nchini Jordan kutoka Jaffa, Falestina katika mwaka wa 1368H (1948) kutokana na vita vilivyopangwa na Mayahudi, La’na ya Allâh iwashukie.

Kukulia Kwake, Kutafuta ‘ilmu Kwake na Waalimu Wake:

Alianza kutafuta ‘ilmu pindi alipovuka kidogo umri wa miaka ishirini. Miongoni mwa waalimu wake waliosifika zaidi alikuwa ni mwanachuoni mkubwa, muhaddith, Sheikh Muhammad Nâsir-ud-Dîn Al-Albânî (*Rahimahullâh*), na kisha mwanachuoni aliyekuwa mmalenga wa lugha ya kiarabu, Sheikh ‘Abdul-Wadûd Az-Zarârî (*Rahimahullâh*), na vilevile wanavyuoni wengine.

Alikutana na Sheikh Muhammad Nâsir-ud-Dîn Al-Albânî kufikia mwishoni mwa mwaka wa 1977 nchini Jordan. Alisoma kitabu cha "Ishkâlât Al-Bâ'ith al-Hadîth" kwa Sheikh al-Albânî katika mwaka wa 1981, na vilevile vitabu vyengine juu ya Madda ya Hadîth na istilahi zake.

Amepata *Ijâzât* (shahada za ta'luma ya dini) katika madda za ki-dini, kwa ujumla na kwa hadîth khususan, kutoka kwa wanavyuoni wengi sana kama vile Shaeikh Badî'-ud-Dîn Shâh As-Sindî (*Rahimahullâh*), mwanachuoni mkubwa, Muhammad Ash-Shanqîtî (*Rahimahullâh*) na wengineo.

Sifa zake kutoka kwa Wanavyuoni:

Wanavyuoni wengi wamemsifu yeye, kama vile:

***Muhaddith*, Sheikh Muhammad Nâsir-ud-Dîn Al-Albânî** (*Rahimahullâh*), ambaye wakati alipokuwa akibainisha kashfa za hasimu wa sunnah, Hasaan 'Abdul-Mannân katika kitabu chake "As-Swahîhah" (2/720), alisema:
"Na kutaka kurefusha katika kuyabainisha maneno yake ya makosa kwenye kuzitangaza ahâdîth zote hizi kuwa ni dha'îf – hili linahitaji yakwamba kuandikwe kitabu khususan kwa ajili hiyo. Lakini wakati wangu hauniruhusu kujiingiza kwenye miradi kama hiyo, kwahivyo labda mmojawapo miongoni mwa ndugu zetu ambao walio wajuzi kwenye ta'luma hii wanaweza kuitekeleza kazi hii, kama vile ndugu yetu 'Alî al-Halabî."

Vilevile rejelea kwenye utangulizi wa Sheikh kwenye kitabu chake "At-Ta'alîqât ar-Raddiyyah 'alâ ar-Rawdat an-Nadiyyah" na "Adâb Az-Zafâf", kilichochapishwa na Al-Maktabah Al-Islâmiyyah, na vilevile kitabu chake "An-Naswîhah."

Sheikh Ibn Bâz (*Rahimahullâh*) vilevile alimsifu na akaandika utangulizi wa kumsifu kwa kitabu chake "Innahâ Salafiyyatul-'Aqîdah wal-Manhaj."
Na vilevile **Sheikh Muhammad Ibn Sâlih Al-'Uthaimîn** na vilevile wanavyuoni wengine wengi wa Saudi Arabia wamemsifu Sheikh 'Alî wakati wa safari yake kwenye ardhi za Makkah na Madînah, ambazo alizosema kwenye darsa yake "Safari yangu ya kuelekea Haramayn" na katika utangulizi wa kitabu chake "At-Ta'rîf wat-Tanbi'ah."
Mwanachuoni mkubwa **Sheikh Muqbil Ibn Hâdî al-Wâdi'î** (*Rahimahullâh*) aliulizwa kwenye kitabu chake "Tuhfatul-Mujîb 'alâ Asilatil-Hadhir wal-Gharîb," Uk. 160: "Unatupendekezea wanavyuoni gani kwa marejeo, kusoma na kuwasikiliza?"
Alijibu: "Tumetangulia kitambo kuyataja hayo, lakini tutayasema tena kwa mara nyengine. Mimi nampendekeza Sheikh Muhammad Nâsir-ud-Dîn Al-Albânî – Allâh amuhifadhi – na wanafunzi wake wa ki-'ilmu kama vile: Ndugu yetu 'Alî Ibn Hasan Ibn 'Abdul-Hamîd, ndugu Salîm al-Hilâlî, na ndugu Mashhûr bin Hasan …" *Rahimahullâh*

Vilevile alisema (*Rahimahullâh*): "Na baada ya hayo niliona kijitabu chenye faida kubwa kiitwacho: Fiqh al-Wâqi' baina an-Nadhariyah wat-Tatbîq (Fiqh ya ukweli baina ya nadharia na

utekelezaji) cha ndugu yetu ‘Alî Ibn Hasan Ibn ‘Abdul-Hamîd; Mimi natoa pendekezo kinunuliwe na kisomwe, twamuomba Allâh amlipe wema (Sheikh ‘Alî Hasan) kwa kazi yake nzuri.”

Vilevile, **Sheikh Muqbil** alikitaja hicho kijitabu kwenye kitabu chake: “Gharatul-Ashritah ‘alâ Ahlij-Jahli was-Safsatah,” na ndani yake akasema: “Kijitabu hiki ni cha kipekee.”
(Sheikh Hussain bin Abdul-Azîz Aal ash-Shaikh (Imâm na Khatwîb wa Masjid an-Nabawî, Madînah, na vilevile ni Hakimu wa Mahkama Kuu ya Madînah – iwapo mpaka sasa hivi 2013 anashikilia nafasi hiyo au ana nafasi nyengine sijui) tarehe 5th Rabî al-Awwal 1422, wakati wa kongamano la QSS Conference iliyofanyika mjini Chicago, Illinois, alisema: “…Sheikh ‘Alî ni ndugu yetu mwandamizi mkubwa, anayetokamana na mjumuiko wa Mashayekh (yeye mwenyewe)... Ama kuhusu Sheikh ‘Alî na Sheikh wake, Sheikh al-Albânî, basi wao ni miongoni mwa wale walioko juu ya manhaj ya Sunnah, na hapana yoyote anayewashuku wao, yakwamba wako juu ya manhaj inayoridhika na kukubalika – na kila sifa njema inamstahiki Allâh... na sheikh ‘Alî ni miongoni mwa wale wanaoitetea manhaj ya Ahlus Sunnah wal Jamâ’ah - kila sifa njema inamstahiki Allâh... **Muheshimiwa Sheikh Abdul-‘Azîz Aal ash-Sheikh ni miongoni wale wanaompenda Sheikh ‘Alî – na mimi najua hili – na anampenda na kumuombea *du’a’*,** na hata pia baada ya Sheikh (‘Alî) kumuona muheshimiwa Sheikh (Sheikh ‘Abdul-Azîz hakupinga yaliyowahi kusemwa kumuhusu yeye hapa). Rudi: QSS Chicago Cassette Tarehe: 20-Jul-01
Sheikh Wasî-Ullâh ‘Abbâs (*Hafidhahullâh*) amesema mnamo tarehe 15 April, 2006: “Sasa hivi hali ilivyo kuhusiana na wanavyuoni wa Jordan, hususan hawa watatu tuliowataja, Sheikh ‘Alî Ibn Hasan al-Halabî, Sheikh Mashhûr Hasan na Sheikh Salîm al-Hilâlî, basi sisi twawajua vilivyo, tumewahi kukaa nao kwenye vikao vingi, tumesikia matamshi yao, tukasoma vitabu vyao, twajua kuhusu imani zao na itikadi zao na twajua yakwamba wao kawaida wanalingania kwenye mazuri na kwenye Sunnah za Mtume (*swallallâhu ‘alayhi wa sallam*) kuhusiana na mas’ala ya ‘aqîdah na vitendo, na hili ni jambo maarufu sana na hakuna yoyote awezae kukataa haya, kwani huu ndio ukweli wa mambo!”
Vilevile, yeye alisema (*Hafidhahullâh*): “Kwahivyo haya ndiyo niliyokuwa nayo ya kusema kuwahusu wanavyuoni wa Jordan, hususan Sheikh ‘Alî Ibn Hasan al-Halabî, Sheikh Mashhûr Hasan na Sheikh Salîm al-Hilâlî. **’Aqîdah zao ni nzuri, Imani zao ziko sawa, na pia wao wako juu ya ‘Aqîdah nzuri**, wao wana ‘ilmu na wamefaidika pakubwa kutokana na hazina kubwa walioachiwa na Imâm al-Albânî na kuwafundisha kuhusu hadîth na riwaya za Mtume (*swallallâhu ‘alyhi wa sallam*). Na wana ‘ilmu tele, hususan kwenye mas’ala ya hadîth...”
“…Na twawanaswihi mufaidike kutoka kwa wanavyuoni wa Jordan kwani wao wamefanya juhudi kubwa katika kujaribu kuisaidia katika kuiimarisha dini ya Allâh kwenye ile miji ambayo da’wah ina haja kubwa ya kuimarishwa. **<u>Na wanavyuoni wengi wamewataja WANAVYUONI wa Jordan kwa uzuri</u>, kama vile Sheikh ‘AbdulMuhsin al-‘Abbâd** (*hafidhahullâh*) ambaye ndiye aliye na ujuzi zaidi katika kuyazungumzia mas’ala haya, na amewataja wao kwa uzuri (Sheikh AbdulMuhsin hakukataa yaliyosemwa kumuhusu yeye hapa).”

(Vile vile katika siku za hivi karibuni, Sheikh ‘Ubaylân, Sheikh ‘Abdul ‘Azîz Rayyis, Sheikh Hamdi ‘Abdul Majîd, Sheikh Ubaykân, Sheikh ‘Abdul Mâlik Ar-Ramadânî, Sheikh Sa’d al-Hussain, wote hao wamemsifu Sheikh ‘Alî)

HAKUNA MWANACHUONI YOYOTE ALIYE-ORODHESHWA AU MATAMSHI YAKE KUTANGAZWA, AMBAO MPAKA LEO WANGALI HAI ALIYEGEUZA SIFA KWA SHEIKH ‘ALI WALA KUSEMA CHOCHOTE CHA UKOSOAJI KUMUHUSU SHEIKH ‘ALÎ.

Juhudi zake kwenye ukumbi wa da’wah:

Alikuwa ni mmojawapo miongoni mwa waanzilishi wa Jarida la Al-Aswâlah, linalochapishwa mjini Jordan, na anahudumu kama mmojawapo wa waandishi na mhariri.

Alikuwa ni mmojawapo wa waanzilishi wa chuo cha “Markaz Imâm al-Albânî” cha Utafiti Wa Ki-ilimu na mafunzo katika Mifumo.

Alikuwa akishughulikia Makala ya kila wiki yaliyokuwa yakichapishwa kwenye Jarida la “Muslimûn” linalochapishwa mjini London na ambalo linalomilikiwa na Jarida As-Sunnah. Chapisho hilo lilidumu kwa muda wa miaka miwili kuanzia tangu mnamo 18th , mwezi wa Rabî’-ul-Awwal 1417H.

Amewahi kuhudhuria kwenye mikutano mbali mbali ya ki-Islamu, Darsa za da’wah na semina za ki-ilimu kwenye sehemu mbalimbali ulimwenguni, kwenye nyakati mbalimbali. Sehemu kama hizo zikiwemo: United States, England, Holland, Hungary, Canada, Indonesia, France na nchi nyenginezo.

Aliwahi kualikwa na Vyuo Vikuu mbalimbali Nchini Jordan ili akatoe mafunzo na kuhudhuria kwenye mikutano kama vile, Chuo kikuu cha Jordan, Chuo kikuu cha Yarmûk, Chuo kikuu cha Zaytûnah, na vyengine vingi.

Vitabu Vyake na Uhakiki:

Vitabu vyake na *Makhtuti* zake alizoziswahihisha zimezidi idadi ya 150, na vinahusu miongoni mwavyo mijalada, vitabu, mijalada ya Magamba magumu, na seti za vitabu. Miongoni mwa vitabu vilivyo muhimu sana alivyotunga ni:

1. ‘Ilm Usûl Al-Bid’ah [‘Imu ya Usûl wa Bid’ah]

2. Dirâsât ‘Ilmiyyah fî Swahîh Muslim.

3. Ru’yatun Wâqi’iyyah fil-Manâhij ad-Da’awiyyah.

4. An-Nukat ‘alâ Nuzhat-in-Nadhar.

5. Ahkâm ash-Shitâ’ fî as-Sunnah al-Mutwahharah.

6. Ahkâm al-‘Eidayn fî as-Sunnah al-Mutwahharah.

7. At-Ta’alîqât al-Athariyyah ‘alal-Mandhûmah al-Bayqûniyyah.

8. Ad-Da’wah ilâ Allâh baina at-Tajammu’ al-Hizbî wat-Ta’âwun ash-Shar’î.

Ama kuhusu Uhakiki wake, basi vitabu vyake vinahusu madda tafauti tafauti, kama vile:

1. “Miftâh Dâr as-Sa’âdah” cha Imâm Ibn Al-Qayyim [Mijalada 3].

2. “At-Ta’alîqât ar-Raddiyyah ‘alâ ar-Rawdhat an-Nadiyyah” cha Al-Albânî [Mijalada 3].

3. “Al-Bâ’ithul-Hadîth” cha Ahmad Shâkir [Mijalada 2].

4. “Al-Hittah fî Dhikri as-Swihâh as-Sittah” cha Sidîq Hasan Khân [Mjalada 1].

5. “Ad-Dâ wad-Dawâ” cha Ibn Al-Qayyim [Mjalada 1].

6. “Al-Mutawârî ‘alâ Abwâb Al-Bukhârî” cha Ibn Al-Munîr [Mjalada 1], na vyengine vingi.

Vitabu vyake vingi vimefasiriwa kwa lugha nyengine, kama vile Kiswahili, Ki-Ingereza, ki-Faransa, ki-Urdu, ki-Indonesia na kadhaalika.

Ref: Imaam Al-Albanee-Center, Jordan

Mfasiri: Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad www.qssea.net

Mkurugenzi wa QSSEA [The Qur’an and Sunnah Society of East Africa]

Makala haya yanatokana kwa hisani ya www.salafibayaan.com